

Kwa hiyo, leo ni siku yako ya kwanza kuwepo nyumbani yako mpya, na...kumbe, hakuna mwanga?

...na simu haifanyi kazi?

Nchini Australia, miliki mingi ipo na mwunganisho wa waya na mabomba kuunganisha na matumizi.

Hii ni pamoja na:

- gesi
- umeme/stima
- laini ya simu
- na maji.

Mengine yanaweza kutofanya kazi mpaka unaanzisha akaunti.

Kabla kuhamia miliki ya kukodisha utahitaji kuwasiliana na watoaji na kupanga kwa matumizi kuunganishwa tena chini ya jina lako.

Kwa mfano, upange kwa umeme na gesi kuwaka au kwa akaunti yako ya simu kuanzishwa na mtoaji siku moja kabla ya kuhamia.

Waweza kuomba ajenti kwa jina la mtoaji na namba yake ya mawasiliano.

Nani analipa kwa matumizi?

Kawaida mpangaji analipa kwa matumizi kama miliki ina mita yake iliyotengwa. Matumizi mengi hayawekwa ndani ya kodi.

Makubaliano ya upangaji uliyowekwa saini pamoja na ajenti na kabaila yanaeleza nani analipa kwa kila tumizi.

Kawaida kuna ada kwa kuunganishwa tena au kuwasha matumizi na mtoaji anaweza kuomba uweke saini kwenye mkataba.

Usiweke saini kwenye mkataba mpya na mtoaji mwingine wa matumizi kabla mkataba wako wa sasa haujakwisha.

Wanaweza kukudai kwa kumaliza mkataba mapema mno.

Vipi kuhusu gesi na umeme?

Miliki mingine ina vijiko na joko vya gesi na gesi kwa kupashajoto

Mingine inatumia umeme.

Wapangaji wanahitaji kulipa kwa utoaji wa gesi na umeme kama miliki ina mita iliyotengwa.

Kama sivyo, huwezi kudaiwa kwa utoaji.

Wasiliana na the Energy & Water Ombudsman Office (Ofisi ya Mchunguzi Maalum ya Nyashati na Maji) kama ukiwa na matatizo na bili zako za gesi na umeme au bishano na mtoaji wa matumizi.

Vipi kuhusu simu, je?

Miliki mingi ina matundu ya kutokea simu. Miliki mingine inaweza pia kuwa na tundu la mtandoni kwa wapangaji kutumia.

Wapangaji wana majukumu kwa gharama zote zinazohusu utoaji na utumiaji wa simu na mtandoni.

Hii ni pamoja na vifaa, gharama za kodi na kuwasha utoaji chini ya jina lako.

Tufanyaje kuhusu TV?

Miliki mingi ipo na kipapasio cha TV lakini wapangaji wanahitaji kutoa TV yao wenyewe.

Kama ukiamua kuongeza huduma mpya, kama TV ya kulipa, hakikisha upate ruhusa kutoka ajenti au kabaila kabla ya kuiweka.

Je, na maji?

Maji ni tofauti na matumizi mengine, yanaunganishwa wakati wote. Kama mabomba hayafanyi kazi, washwa maji kutoka mwunganisho ya mita.

Ulipe tu kwa matumizi yako ya maji kama miliki ina mita ya maji iliyotengwa. Kawaida nyumba zina mita ya maji iliyotengwa.

Lakini gorofa ni tofauti. Magorofa mengi yana mita ya kushirikiana. Kabaila analipa kwa maji kwa sababu hakuna mita iliyotengwa.

Kama una mita iliyotengwa, lazima ajenti akutumia nakala ya billi ya maji kuonyesha matumizi yako ya maji.

Ajenti au kabaila akupe nakala ya bili katika miezi mitatu na akupe angalau siku 21 za kuilipia.

Lazima wapange mwunganisho wa 'maji ya kufaa' kama vichwa vya manyunyuni kuokoa maji na kutengeneza mabomba yenye mvujo ili kuokoa maji na pesa.

Kama matumizi yoyote yanavunjika wasiliana na ajenti au kabaila yako mara moja ili yatengenezwa.

Kwa mfano, kama bomba la maji linavunjika, unahitaji kufahamisha ajenti au kabaila mara moja.

Aina hiyo ya utengenezaji ni 'utengenezaji wa haraka' chini ya masheria ya upangaji na lazima utengenezwe kwa haraka.

Kama huwezi kuwasiliana na kabaila au ajenti au wasipotengeneza tatizo katika muda uliofaa, waweza kupanga kwa fundi wenye sifa zinazostahili kutatua tatizo na umlipia wewe mwenyewe.

Waweza kupata pesa zako kurudishwa na kabaila katika siku 14 –

- kama kazi ni chini ya \$1,000
- hakusababisha hasara
- ulimpa kabaila au ajenti nafasi ya kufaa kutengeneza tatizo
- una risiti na taarifa iliyoandikwa ya tatizo kutoka fundi wenye sifa zilizostahili.

Kama huwezi kulipa kwa utengenezaji wewe mwenyewe, waweza kuomba Consumer, Trader and Tenancy Tribunal (Mahakama ya Mtumiaji, Mwenye biashara na Upangaji) kwa agizo kwa kabaila kutengeneza tatizo.

Kupata maelezo zaidi kuhusu haki na majukumu ya wapangaji, tembelea tovuti ya Fair Trading kwa www.fairtrading.nsw.gov.au au piga simu namba ya 13 32 20.

Kama ukihitaji msaada wa lugha pigia simu 13 14 50.